The Management University of Africa | MUA
Sponsored by the Kenya Institute of Management

# UNDERGRADUATE UNIVERSITY EXAMINATIONS

## SCHOOL OF MANAGEMENT AND LEADERSHIP

## DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION ARTS

**KIS 214 :** **FONETIKI NA FONOLOJIA**

**DATE:** **2ND APRIL 2026**

**MUDA:** Saa 2

**JUMLA YA ALAMA:** 70

**MAELEKEZO:**

1. Andika **nambari yako ya usajili** kwenye kijitabu cha majibu.
2. **USIANDIKE** chochote kwenye karatasi hii ya maswali.
3. Karatasi hii ina **maswali sita (6)**.
4. **Swali la KWANZA ni la lazima.**
5. Jibu **maswali mengine matatu (3)** yoyote.
6. **Mgawanyo wa alama:**
7. Swali la KWANZA lina alama **25**
8. Maswali mengine yana alama **15 kila moja**
9. Andika majibu yako yote kwenye **kijitabu cha majibu** ulichopewa.

**SWALI LA KWANZA**

a. Kwa kutumia mifano mwafaka, tofautisha dhana zifuatazo:-

i. Toni na Tonisho **(Alama 3)**

ii. Silabi wazi na Silabi funge **(Alama 3)**

b. Onyesha sifa bainifu za utamkaji wa foni hizi:- **(Alama 9)**

i. [ ʤ] ii. [ ɔ ] iii. [ ʃ ]

c. Bainisha matawi matatu makuu ya fonetiki **(Alama 6)**

d. Fafanua aina mbilli kuu za fonolojia **(Alama 4)**

**SWALI LA PILI**

a) Yanukuu maneno yafuatayo kifonetiki:- **(Alama 9)**

i. Nyoosha

ii. Chanzo

iii. Dhoruba

b). Onyesha sifa bainifu zinazozingatiwa katika uanishaji wa irabu kimatamshi.

**(Alama 6)**

**SWALI LA TATU**

a). Tofautisha kati ya ala tuli na ala sogezi. **(Alama 3)**

b). Kwa kurejelea mkondohewa nje, eleza jinsi binadamu huzalisha foni za lugha.

**(Alama 12)**

**SWALI LA NNE**

a**).** Fafanua dhana ya mifanyiko ya kifonolojia **(Alama 3)**

b). Fafanua jinsi mifanyiko ifuatayo ya kifonolojia hutokea katika lugha ya

Kiswahili **(Alama 12)**

i. Udhoofikaji wa konsonanti

ii. Unazalishaji pamwe wa nazali

iii. Uimarikaji wa konsonanti

iv. Tangamano la irabu

**SWALI LA TANO**

a). Bainisha tofauti kati ya muundo wa silabi na umbo la silabi **(Alama 3)**

b). Silabisha neno SEKTA **(Alama 4)**

c) Changanua umbo la kila silabi katika neno JADHBA **(Alama 8)**

**SWALI LA 6**

a). Tumia mifano mwafaka kufafanua dhana zifuatazo:- **(Alama 5)**

i. Fonimu

ii. Alofoni

b). Pambanua mbinu nne zinazotumia kudhihirisha kuwepo au kutokuwepo kwa fonimu na alofoni katika lugha ya Kiswahili. **(Alama 10)**